

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS –TAMISEMI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO**

SHULE YA SEKONDARI MDANDO,  
S.L.P 179,  
**LUSHOTO**  
15.12.2020

**KUMB Na: MDSS/JI16/F1/2021**

**JINA LA MWANAFUNZI**

.....

**YAH: KUCHAGULIWA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021 MDANDO SEKONDARI**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule ya secondary **MDANDO**. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021**. Ni matumaini yangu kuwa utaitumia vema nafasi hii adhimu uliyopewa na serikali.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA WAKATI WA KURIPOTI SHULENI**

**1. SARE ZA SHULE:**

**WASICHANA**

- (i) Sketi mbili za rangi ya **LIGHT BLUE(bluu bahari)** zinazovuka magoti.
- (ii) Mashati mawili nyeupe ya mikono mifupi, kwa waislamu wanaruhusiwa kushona nusu kanzu nyeupe ya mikono mirefu na hijabu nyeupe isiyo na urembo wa aina yeyote.
- (iii) Soksi nyeupe jozi mbili au zaidi kwa usafi binafsi.
- (iv) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi vya kufunga kwa kamba, na SIO RABA au BAJAJI
- V) T-shirt moja rangi ya kijivu yenye nembo ya shule kwa ajili ya michezo na kazi za shamba.
- Vi) Sweta rangi ya grey(kijivu ) lenye umbo la "V" kwenye shingo na lenye nembo ya shule kwa ajili ya baridi.

**WAVULANA**

- (i) Suruali mbili rangi ya GREY(kijivu) zisizobana.
- (ii) Mashati mawili rangi nyeupe ya mikono mifupi.
- (iii) Soksi nyeusi jozi mbili au zaidi kwa usafi binafsi.
- (iv) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi vya kufunga kwa kamba, na SIO RABA.
- v) T-shirt moja rangi ya grey(kijivu) yenye nembo ya shule kwa ajili ya michezo na kazi za shamba.
- Vi) ) Sweta rangi ya grey(kijivu) na yenye shingo ya umbo la "V" kwa ajili ya baridi.

## **2. VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

- Madaftari aina ya Counter books **kumi na moja (11) QUIRE 2 AU 3.**
- Dictionary (Kamusi inayotafsiri maneno ya kiingereza kwa kiswahili kwa matumizi yake binafsi na kujifunza lugha ya kiingereza.
- Kalamu za wino pamoja na penseli.
- Mkebe wa vifaa vya kujifunzia hisabati (mathematics) pamoja na jiografia.

## **3. VIFAA VYA USAFI NA ELIMU YA KUJITEGEMEA**

- i. Fagio moja la chelewa kwa ajili ya usafi wa mazingira kwa wasichana.
- ii. Ndoo 1 yenye mfuniko kwaajili ya kuhifadhi maji ya kupikia chakula cha wanafunzi.
- iii. Jembe au kwanja 1 kwa ajili ya usafi wa mazingira kwa wavulana.
- iv. Sahani moja, kijiko na kibakuli kwa ajili ya chakula.

## **4. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA /KUFUKUZWA SHULE.**

- a) Uasherati, ubakaji na ushoga, kuoa au kuolewa.
- b) Wizi, ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
- c) Kuvuta bangi.
- d) Kupiga au kupigana.
- e) Kudharau Bendera ya Taifa, kuharibu mali ya umma.
- f) Kupata, kutoa mimba au kusababisha mimba shuleni au nje ya shule.
- g) Kugoma, kuongoza, kuchochea mgomo au vurugu, kuchafua amani au usalama wa watu.
- h) Kukashifu au kukataa adhabu halali.

### **Angalizo.**

1. Ni jukumu la mwanafunzi kufuata sheria na taratibu zilizowekwa pamoja na nyingine ili kuepuka adhabu na kufukuzwa shule.

Walimu shuleni ni waelekezaji, walezi, waelimishaji na washauri. Mwanafunzi akiwasikiliza, atafika kule anakotarajia, alikopanga afike.

2. Ni matumaini yangu kuwa utajituma zaidi kwenye masomo ili kujipaisha kitaaluma wewe mwenyewe binafsi pamoja na shule kwa ujumla.
3. Lugha ya mawasiliano shuleni ni KIINGEREZA hivyo hatua kali zitachukuliwa dhidi ya atakayekiuka agizo hili.
4. Kutakua na wiki sita kwa ajili ya kujifunza lugha ya KIINGEREZA.

## **CHAKULA**

Kutokana na agizo la serikali la kutoa chakula cha mchana kwa kila shule, makubaliano yameafikiwa kwenye kikao cha wazazi kwa kila mzazi kuchangia kama ifuatavyo:-

1. Debe mbili za mahindi(kilo 40) kwa mwaka; (inaweza kulipwa kilo 20 kwa muhula)
2. Maharage kilo 4( kwa mwaka)
3. Tsh 6000/= kwa ajili ya kusaga/kukoboa na mpishi.

## **5. PAMOJA NA BARUA HII UNATAKIWA KUKAMILISHA /KUJAZA VIAMBATISHO "A" NA "B" VIFUFUATAVYO:-**

- i. Medical examination form itajazwa na mganga katika hospitali ya serikali na itarudishwa shuleni ikiwa imejazwa kikamili sikufu ya kuripoti.
- ii. Fomu ya kukubali kujiunga na shule ya sekondari Rangwi.
- iii. Viambatisho vyote vinapaswa kujazwa kikamilifu na kurudishwa shuleni siku ya kuripoti shuleni.

**KARIBU SANA MDANDO SEKONDARI**

.....  
**HASSANI S. FERUZI**  
**MKUU WA SHULE**  
**0682615103/0717002928/0621249323**

**KIAMBATANISHO A.**

The united Republic of Tanzania  
Presidents' office, regional administration and local government.

MDANDO SECONDARY SCHOOL,  
P.O.BOX 179,  
**LUSHOTO.**  
**12/12/2020.**

Ref. No. **MDSS/JI/ F1/2021**

To the Medical Officer

.....  
.....

**RE: STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION FORM**

Please examine the student

..... In  
respect of these areas and any other area (s) deemed fit please. Delete whichever not  
applies.

Does the student have problems in connection with?

a) Sight. Yes/ No. If yes, state

.....  
.....  
.....  
.....

b) Hearing. Yes/No. If yes, state

.....  
.....  
.....  
.....

Any other problem identified, please state

.....  
.....  
.....

Do you therefore recommend this student to pursue studies at this school?

.....  
.....

Name ..... signature .....

Date .....

Official title ..... Official stamp.....

## KIAMBATISHO B

Anuani .....

S.L.P. ....

Tarehe .....

Mkuu wa shule,  
Shule ya sekondari Mdando,  
S. L. P. 179,  
LUSHOTO.

### YAH. KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE HII

Asante kwa barua yako ya tarehe 15/12/2020.

- a) Nakubali / sikubali nafasi niliyopewa ya kidato cha kwanza mwaka 2021.
- b) Niko tayari / siko tayari kufuata sheria, maagizo na masharti ya mdando sekondari.
- c) Nitahudhuria / sitahudhuria masomo yote ninayotakiwa kusoma hapa shuleni.
- d) Nikishindwa kuhudhuria bila ya sababu za msingi nifukuzwe shule au hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

.....  
Jina na sahihi ya mwanafunzi

.....  
Jina na sahihi ya mzazi / mlezi

## KIAMBATISHO B

Anuani .....

s. l. p. ....

Tarehe .....

Mkuu wa shule,  
Shule ya sekondari mdando,  
S. L. P. 179,  
LUSHOTO.

### YAH. KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE HII

Asante kwa barua yako ya tarehe 15/12/2020

- a) Nakubali / sikubali nafasi niliyopewa ya kidato cha kwanza mwaka 2021.
- b) Niko tayari / siko tayari kufuata sheria, maagizo na masharti ya mdando sekondari.
- c) Nitahudhuria / sitahudhuria masomo yote ninayotakiwa kusoma hapa shuleni.
- d) Nikishindwa kuhudhuria bila ya sababu za msingi nifukuzwe shule au hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

.....  
Jina na sahihi ya mwanafunzi

.....  
Jina na sahihi ya mzazi / mlezi